



Penn Manor  
School District

Jamii iliobora...mwanafunzi mmoja mmoja

## WILAYA YA SHULE YA PENN MANOR

S.L.P 1001 • Millersville, PA 17551-0301  
simu (717) 872-9500 • Faksi (717) 872-9505  
[www.pennmanor.net](http://www.pennmanor.net)  
Muajiri wa fursa sawa

Michael G. Leichliter, Ed.D.

Mwelekezi

[mike.leichliter@pennmanor.net](mailto:mike.leichliter@pennmanor.net)

Machi 2, 2020

Kwa wazazi na Walezi,

Wilaya ya shule ya Penn Manor ni aminifu kwa afya na usalama ya wanafunzi na wafanyikazi wetu. Wilaya ya shule inafuatilia kwa umakini ujumbe unaohusiana na virusi vya Corona COVID-19. Tunavyofanya kwa kila kesi za kiafya, tunashirikiana kwa ukaribu na kupokea uelekezi wa ziada kutoka Idara ya Afya ya Pennsylvania (DOH), vituo vya kukabiliana na kokinga kutokana na magonjwa (CDC), na daktari wetu wa wilaya ya shule.

*Tafadhali zingatia: hakuna visa vyovoyote vya virusi vya corona vilivyopotiwa kwa wilaya yetu ya shule.*

Tunapeana ujumbe huu kwako ili uwe na ufahamu kuhusu swala hili na uhakika kuwa wilaya yetu inamipango tayari ya kufuatilia, kujitayarisha, na kuajibika kwa swala lolote la kiafya au kiusalamu linaloweza kutukumba. Pia tunawahimiza kutumia [Vituo vya Kukabiliana na Ugonjwa \(CDC\)](#) na [Idara ya Afya ya Pennsylvania \(DOH\)](#) kama rasilimali zinazoaminika kwa taarifa za punde na uelekezi kuhusu swala hili ya kiafya.

Ni azimio la wilaya ya shule kufanya kile kinawezekana kusaidia kokinga kusambaa kwa virusi hivyo kutapokuwa na mkurupuko kwa eneo hilo, **na tunahitaji msaada wako kufanya hivi.**

Idara ya Afya ya Pennsylvania imewasilisha jinsi zifuatazo kwa tovuti yake kusaidia kuzuia kusambaa kwa virusi vya kupumuliwa, kama vile COVID-19:

- **Funika** kohozi yejete au unapopiga chafya ukitumia tishu kisha utupe tishu hio kwenye pipa; kama kuna ukosefu wa tishu, kohoa au piga chafia ndani ya kisigino chako. Usitumie mikono yako.
- **Nawa mikono** kwa sabuni na maji kwa angalau sekunde 20. Tumia kemikali ya kusafisha mikono ilio na ethanol kama sabuni na maji hazipo.
- **Safisha** sakafu kila mara, kama vile sakafu za kazi, mitambo ya kuzima na kuwashaa taa, rununu na mahali panapoguswa sana.
- **Punguza** uwezekano wa kusambaa. Kama unaugua, kaa nyumbani hadi upate nafuu. Usitangamane na watu ambaa wanaugua tayari.

Wilaya ya shule ya Penn Manor School inafuatilia kisa hiki kwa umakini (sio virusi vya corona pekee lakini pia homa iliokuwa mwaka huu) na inasafisha na kuondoa maradhi shulenii kila siku kama moja ya

Huduma za kikastodia zinazoendela. Kunapokuwa na visa vilivyodhibitishwa vyatika COVID-19 kwa eneo hio, wilaya ya shule itafuata maelekezo yaliyopeanwa na wataalam wa kiafya kuhusu hatua za ziada ambazo ni muhimu.

Kama mtoto wako ataugua, tafadhali fuata maelekezo haya kuhusu magonjwa ya wanafunzi:

1. Mtoto wako anapaswa kuwa huru kutokana na homa kwa saa 24, bila matibabu, kabla ya kurudi shulenii.
2. Watoto wanao tapika na kuhara lazima awekwe nyumbani kwa saa 24 baada ya kipindi cha mwisho.
3. Watoto wanaoshukiwa kuwa na magonjwa ya kuambukizwa (kama vile macho waridi na upele usiojulikana) wanapaswa kuwekwa nyumbani hadi dhibitisho kutoka kwa mhudumu wako wa kiafya lipokewe.
4. Kama mtoto wako ni mgonjwa, mueke nyumbani, bila kuzingatia ziara nyanjani, parties or other special events that may be held at school that day.

Ni muhimu kwa sasa tukishirikiana pamoja ili kumakinika kwa kile tunaweza kukabiliana naycho. Tutuakuwa waangalifu kwa kufuatilia hali ya magonjwa yote ambayo yanaweza kutisha wanafunzi na wafanyikazi wetu.

Asante kwa kuunga mkono wilaya yetu, shule zetu, wafanyikazi wetu, na wafanyikazi wetu.

Wako mwaminifu,



Michael G. Leichliter, Ed.D.  
Mwelekezi wa Shule